Gazeti la kwanza la Islam kutolewa kwa lugha ya Kiswahili - mwaka 1936

Mapenzi ya Mungu

Mapenzi kwa wote bila chuki kwa yeyote

DAR ES SALAAM TANZANIA

JUZU 81 No. 219 | JAM.I-RAJ 1442AH | JAN-FEB 2021 | TABLIGH 1400 HS | BEI TSH. 500/=

Nukuu ya Qur'an Tukufu

Hakika watu wanaomkurubia zaidi Ibrahimu ni wale waliomfuata yeyena Mtume huyu na walioamini; na Allah ndiye mlinzi wa waaminio.
Surah 3:69

Maisha ya Mtume Mtukufu Muhammad saw

Inaendelea Kutoka toleo lililopita

Yalivyosimuliwa na Hadhrat Mirza Bashir ud Din Mahmud Ahmad r.a. Khalifatul Masih wa pili wa Masihi Aliyeahidiwa as

KUMWABUDU MUNGU NDANI YA PANGO LA HIRA

Umri wa Mtume saw. ulipozidi miaka thelathini, basi moyo wake ukaelekea zaidi kwenye ibada ya Allah kuliko hapo awali. Hatimae baada ya kuchukizwa na utukutu, maovu na uharibifu wa watu wa mjini, basi akaelekea nje ya Makka kwa umbali wa maili mbili au tatu hivi, kwenye kilele cha mlima fulani ndani ya kijipango fulani cha mawe na kuanza kufanya ibada ya Allah. Hadhrat Khadija r.a. alikuwa akimtayarishia chakula cha siku chache. Alikuwa akikichukua na kwenda kwenye pango la Hira na kukaa ndani ya mawe hayo mawili au matatu na kujishughulisha usiku na mchana katika kumuabudu Allah.

WAHYI WA KWANZA WA KURANI

Siku moja, alipokuwa na umri wa miaka arobaini, aliona mandhari Fulani ya Kashfi wakati akiwa ndani ya pango hili hili, kwamba mtu Fulani akimwambia: "Soma!" Akajibu: "Mimi mbona sijui kusoma." Hapo akamwambia tena kwa mara ya pili na ya tatu na



hatimae akamsemesha sentensi tano zisemazo:

Soma kwa jina la Mola Wako Aliyeumba. Alimwumba mwanadamu kwa tone la damu iliyoganda. Soma! Na Mola Wako ni mwenye heshima kuliko wote. Ambaye Alifundisha kwa njia ya kalamu. Alimfunza mwanadamu Asiyoyajua.

Huu ndio ule Wahyi wa mwanzo wa Kurani ulioteremka kwa mtume wa Mungu, Muhammad saw. Mradi wake ni huu kwamba soma ujumbe wa kimbingu uwasikilizishe dunia nzima, kwa jina la Mola Wako Aliyekuumba wewe na viumbe wote wengine. Mungu Yule Aliyemuumba mwanadamu kwa njia hii kwamba hupatikana ndani ya moyo wake (huyo mwanadamu) mbegu ya upendo wa Allah na viumbe Vyake. Naam, wasikilizishe wote duniani ujumbe huu kwamba Mola Wako, Mwenye kuheshimika kuliko wote Atakuwa pamoja nawe. Aliyeiumba kalamu kwa ajili ya kuifundisha dunia elimu mbali mbali na Akawa tayari kumfundisha mwanadamu kile ambacho (mwanadamu) hakukijua hapo kabla.

Maneno haya machache, yameyazunguka mafundisho yote yale ya Kurani yaliyokuwa yaje kumteremkia Mtume Muhammad saw. na ndani yake mlikuwa mnapatikana mbegu fulani muhimu ya urekebishaji wa dunia hii. Maelezo yake yatakuja kwa wakati muafaka ndani ya Kurani Tukufu. Aya hizi zimeelezwa hapa kwa sababu hii tu kwamba hili ni tukio muhimu la maisha ya Mtume Mkarimu saw. na aya hizi zinakuwa kama jiwe la msingi la Kurani Tukufu.

Maneno haya yalipomteremkia Mtume Muhammad saw., basi moyoni mwake mkawa na hofu hii kwamba: Je nitaweza kulitekeleza jukumu kubwa la aina hii la Allah? Kama ingekuwa ni mtu mwingine, basi akili yake ingeharibika kutokana na kiburi na majivuno kwamba Mungu AmeMkabidhi kazi Fulani. Lakini mtume wa

Endelea uk. 5

Jamia Ahmadiyya yapiga hatua 2020

Na **Juma Iddy Abeid**
Kigoma

Alhamdulillah, kwa fadhili za Allah na kwa Baraka za maombi maalum ya Hazrat Khalifatul Masihil Khaamis atba, kwa mara nyingine tena leo tumekutana katika hafla hii adhwiim ya kuwaaga vijana wetu wanaohitimu Jamia Ahmadiyya, ambayo ni moja ya taasisi muhimu sana zilizoanzishwa na Mtukufu Hazrat Masihil Mau'ud a.s katika mwaka wa 1906, imekuwa ikitoa mchango mkubwa sana katika ustawi na maendeleo ya Jamaat ulimwenguni kote. Pamoja na majukumu ya kimasomo, wakufunzi na wanachuoni wa taasisi hii wamekuwa wakishiriki vyema



Wahitimu wa Jamia Ahmadiyya 2020 (mbeleni) pamoja na Amir na Mbashiri Mkuu na wakufunzi wa chuo katika picha ya pamoja

katika majukumu mbalimbali ya Jamaat kama vile mahubiri, michango nk.

KUTOA MICHANGO KATIKA NJIA YA ALLAH

Kwa upande wa michango, wakufunzi na wanafunzi wote wameshiriki kikamilifu katika uwanja huu. Na kwa msaada wa Allah tumefanikiwa kutimiza ahadi zetu za Tahrik e Jadeed na Waqfu Jadeed na kukamilisha na kuvuka bajeti yetu ya mwaka mzima, ambapo zaidi ya Tsh 20,000,000/= (milioni ishirini) zimechangwa Alhamdulillah.

TABLIGH (MAHUBIRI)

Pamoja na changamoto ya Corona

Endelea uk. 2

Unataka Kuanza Biashara? uk. 4

Mapenzi ya Mungu

Maoni ya Mhariri

UGUMBA WA KIROHO

Huzur atba alisema kwamba:

"Kwa kuwa hakuna atakayefurahi kwamba ndoa za miaka mingi zikatae kuzaa matunda ya mimba, hivyo hali ambapo Waislamu wengi Waahmadiyya wanakuwa hawawezi kupata Baiat kwa kuwaingiza watu ndani ya Jumuiya sio hatua ya kukaribishwa. Kwa hiyo kila mmoja ni lazima ajitahidi, kama ifanyikavyo kimwili, ili kuepukana na ugumba wa kiroho. Muwe na uchungu pale yeyote miongoni mwenu aonapo vigumu kupata Baiat kwani huo ni ugumba wa kiroho ambao mnatakiwa mjitahidi kuondokana nao pamwe na kutoa sadaka za mara kwa mara, kufunga saumu na kusujudu kwenye kizingiti cha Allah.

"Kwa kuwa kila mmoja ataulizwa mbele ya Allah, kiwango cha chini kabisa cha shukrani ambacho mtu anaweza kukitoa kwa Allah katika kuongoza kwenye nuru ya Ahmadiyya ni kuieneza nuru hiyo kwa wengine kwa kujihusisha sana na shughuli za Tabligh kwa mapana na marefu. Wale wenye kuzikalia habari hizo nzuri (za kuwafikishia watu ujumbe wa Ahmadiya) ni aidha wabinafsi au waoga."

Pia Huzur atba alibainisha mbinu zitakazomsaidia kila mtu katika kuwaita watu kwa Allah pale aliposema:

1. Ni dhamira ya kuwafikia na ujumbe wa Islam asilimia hamsini ya watu walioko kwenye maeneo yote. Uwasilishaji uwe ni mzuri kuhakikisha uamuzi na hatua za haraka katika kuwasiliana na wanaohubiriwa.
2. Kila mwanajumuiya, kila nyumba na kila Jamaat wapewe lengo la Baiat. Masuala ya Tabligh yawe ndio ajenda za mwanzo kabisa katika ngazi zote. Ziara zote za viongozi zizingatie jambo hili.
3. Sauti ya Jamaat ni lazima isikike kwa nguvu na uwazi kabisa katika kila jambo lenye maslahi ya Kitaifa.
4. Machapisho ya kukabiliana na kila aina ya propaganda na utovu wa uadilifu dhidi ya wanadamu yawe yakitolewa kwa haraka iwezekanavyo.

Jamia Ahmadiyya Yafana zaidi 2020

Kutoka uk. 1

kuathiri kwa kiasi kikubwa utendaji wa shughuli zetu za mahubiri hususan katika miezi ya Machi, Aprili, Mei na Juni ,hata hivyo jitihada maalum zilifanyika ili kufanikisha jukumu hili. Jitihada hizo ni kama vile fursa yetu ya sabasaba, tabligh day nk. Ambapo zaidi ya vipindi 20 shughuli zilifanyika na vipeperushi zaidi ya 4000 (elfu nne) viligawiwa, watu zaidi ya 47000 walihubiriwa na mauzo ya vitabu vyenye thamani ya zaidi ya Tsh 2,000,000/= (milioni mbili) viliuzwa Alhamdulillah. Zaidi ya hayo, kwa mara ya kwanza katika historia yetu ya Jamia, mwaka huu katika sherehe za wakulima al-maarufu Nanenane, taasisi yetu ya Jamia tuliweka banda letu maalum na kazi ya mahubiri ilifana sana katika banda hilo. Watu wengi walifika hapo kuangalia na kununua vitabu, kuuliza maswali na hata kufanya ibada pia.

WAQAR-E-AMAL – KAZI ZA KUJITOLEA

Miongoni mwa majukumu yetu ni kufanya kazi mbalimbali za kujitolea – yaani Waqar e amal, ambapo jumla yake ni 90 (tisini) na jumla ya fedha iliyookolewa ni zaidi ya Tsh. 4,500,000/=

KILIMO CHA BUSTANI YA MATUNDA NA MBOGAMBOGA

Tangu miaka kadhaa iliyopita tulikuwa na bustani ya matunda tu pekee, lakini katika huu mwaka wa 2020 tumeongeza bustani ya mboga za aina mbalimbali kama vile Maharage, kunde, kabeji, sukuma wiki, mchicha, biringanya, bamia n.k. Na kupitia bustani hizi wanachuo wamepata manufaa makubwa sana, ikiwemo pia kuokoa kiasi cha fedha takriban Tsh.2,000,000/= (milioni mbili). Na miongoni mwa faida hizo ni kutembelewa na wanafunzi na wahadhiri wa kutoka vyuo mbalimbali ambao pamoja na mengine pia walitoa ushauri wa kitaalamu jinsi ya kuboresha zaidi bustani hizo.

M.T.A

Kwa upande wa MTA, wanachuo hushiriki kikamilifu katika kusikiliza na kutazama hotuba za Huzoor atba katika siku za Ijumaa nk. Nayo ni lazima kwa kila mwanachuo kutazama hotuba za Ijumaa bila ya kukosa. Na kwa njia hii mawasiliano baina ya Khalifa atba na wanachuo yanazidi kuboreka.

VIKAO VYA WAFANYAKAZI

Ili kuboresha utendaji wa kazi, uongozi wa chuo yaani mkuu wa chuo, masheikh na walimu wote wamekuwa wakifanya vikao mara kwa mara. Na miongoni mwa vikao hivyo, vipo vile vya kawaida ambavyo hufanyika kila Jumapili ya mwanzo wa mwezi, vikao vya kujadili matokeo ya mitihani yaani result meeting, vikao vya dharura nk.

DARASA LA TEHAMA

Darasa la TEHAMA limekuwa likiendelea vizuri ambapo wanafunzi wote wa mwaka wa mwisho hufundishwa elimu ya matumizi ya kifaa hiki muhimu hususan katika zama hizi za maendeleo ya kisayansi na teknolojia ili nao wasibaki nyuma katika uwanja huu.

KAZI ZA SHULENI

Kwa upande wa Shule yetu ya msingi, Masheikh na baadhi ya waalimu wamekuwa wakijitolea kutoa huduma mbalimbali kama vile kuimarisha nidhamu ya wanafunzi, kutoa elimu ya dini nk.

SEMINA ZA MALEZI KIMADARASA

Kila Jumapili ya pili ya katika mwezi, hufanyika semina katika madarasa yote. Mada mbalimbali hupangwa kutoka katika kikao cha wafanyakazi na kila Sheikh na mwalimu wa madarasa husika huziwasilisha na kuzifafanua kwa wanafunzi madarasani. Matokeo ya semina hizi huwa ni yenye faida kubwa kwa walengwa. Zaidi ya hayo, ndugu yetu Mzee A.R. Mikila sahib anajitolea kuwafundisha vijana elimu ya maelezo ya Qurani Tukufu, darasa hili analiendesha mara moja kwa kila mwezi na wanafunzi wanafaidika sana kwalo.

MAPOKEZI NA USAJILI KWA WANAFUNZI WAPYA

Kila mwaka ifikapo mwezi Januari, tunapokea wanafunzi wapya, na mara baada ya kuwapokea, tunawafanyia usaili kwa kuwatolea mitihani ya kuwapima na wale wanaokidhi vigezo hupata nafasi ya kuanza masomo.

SEMINA JUU YA TARATIBU ZA HOSTELI

Semina mbalimbali hutolewa zinazohusu miiko, kanuni, taratibu na miongozo ya Hosteli. Kazi hizi hufanywa na Masheikh na Waalimu wasimamizi wa Hostel.

ZAWADI YA IDI-E-L FITR KWA WASIOJIWEZA

Kwa upande wa sherehe za Iddi elftr, idara yetu ya Jamia Ahmadiyya tumetoa zawadi ya mchele, unga, sabuni nk. Kwa wananchi wasiojiweza kutoka katika mitaa ya Msamvu B, Ngerengere na Kitata. Takriban familia zipatazo mia moja zimefikiwa na msaada huo.

Pia katika sherehe za Iddi el-Hajj, idara yetu imefanikiwa kugawa dhabihu kwa kaya zipatazo 170 zinazotuzunguka. Taarifa hizi zote zilirushwa hewani kupitia Abood Radio na Abood Tv.

MAOMBI MAALUM KWA AJILI YA HUZOOR (A.T.B.A)

Kufuatia mkasa uliomkuta Hazrat khalifatul Masihil khaamis atba kwa kuanguka na kujeruhika, wanachuo tuliguswa sana na tukio hili, hivyo tulifanya maombi maalum kwa ajili yake na pia kutoa dhabihu.

SEMINA JUU YA IMANI YA UCHAWI

Endelea uk. 3

BODI YA UHARIRI

Msimamizi: Sheikh Tahir M. Chaudhry - Amir Jamaat, Tanzania.
Mhariri: Dr. Swaleh Kitabu Pazi
Kompyuta: Ahmad Abdul Nasibu.
Mchapishaji: Sheikh Bashart Ur Rehman
Msambazaji: Mwl. Omari Ali Mnungu
Wajumbe:
1. Mwl. Abdullah Khamis Mbanga
2. Mahmood Hamsin Mubiru.
3. Jamil Mwanga.
4. Abdillah Kombo

Makao Makuu - Ahmadiyya Muslim Jamaat Tanzania,
Mtaa wa Bibi Titi Mohammed, S.L.P. 376.
Simu 022 - 2110473, Fax 022 - 2121744, Dar es Salaam, Tanzania.
Email: mapenziyamungu36@gmail.com

Jamia Ahmadiyya yapiga hatua 2020

Kutoka uk. 2

Kutokana na kushamiri sana imani za kishirikina katika jamii na hasa imani za kichawi, kurogwa nk. ambapo hata baadhi ya waislamu na hasa walio wengi huamini mambo haya, uongozi wa taasisi yetu ulichukua hatua maalum wa kutoa hotuba madarasani, kufanya semina ya pamoja msikitini ambapo Masheikh na waalimu walitoa hotuba za kubatilisha imani hizo kwa hoja madhubuti ushahidi wa kimazingira na uzoefu wao katika jamii juu ya jambo hili. Na kisha wanafunzi walisomewa waraka maalum kutoka kwa Hazrat Khalifatul masihil khaamis atba ulioelezea na kujibu shutuma za uchawi uliofanywa dhidi ya Mtume^{saw}, waraka huo walisomewa kila siku asubuhi mstarini mara baada ya usomaji wa Qurani Tukufu na tafsiri yake.

SIKU YA MICHEZO-SPORTS DAY

Ama inavyofahamia, wanafunzi wetu hushirikishwa katika mashindano mbalimbali ya kimwili na kielimu. Mashindano ya kimwili hufanyika katika muhula wa kwanza na ya kielimu hufanyika katika muhula wa pili.

Kuna timu tatu zinazoshiriki mashindano ya kimwili ambazo ni Amanat, Shafkat na Shujaat. Mashindano huanzia katika hatua za awali na mwisho hufanyika fainali katika siku maalum yaani Sports day.

Miongoni mwa michezo mipya ni "Barry" ambao umeanzishwa mwaka huu, mchezo huu umekuwa kivutio kikubwa wa washiriki na watazamaji pia.

MIHULA YA MASOMO KATIKA MWAKA

Kuna mihula miwili ya masomo katika mwaka, muhula wa kwanza huanza mwezi wa Januari na kuishia mwezi Juni na muhula wa pili huanzia mwezi Julai na kuishia mwezi Disemba. Mwishoni mwa kila muhula inafanyika mitihani, na wale wanaofaulu katika mitihani yote ya mihula miwili wanasonga mbele na uingia katika madarasa mapya. Na ama wale wanaofeli kuanzia mitihani mitatu na zaidi wanarudia madarasa◎

Katika miezi ya likizo wanafunzi wanatumwa waqfu ardhi na huleta ripoti mara wanaporudi kutoka huko. Taarifa zinaonyesha kuwa mpango huu umekuwa ukitoa matokeo mazuri. Na katika mwezi uliopita wa kumi na mbili takriban wanafunzi 16 walienda Waqfu Ardhi.

KUPELEKA WANAFUNZI NCHINI GHANA

Kwa fadhili za Allah, kila mwaka chuo chetu hupata nafasi mbili za kupeleka wanafunzi nchini Ghana kwa masomo ya juu ya ubashiri, na hata mwaka huu wa 2020 tunao vijana wawili ambao wapo tayari kwa safari ya kuelekea huko na michakato yote imeshakamilika, hivi sasa wanasubiri ruhusa ya serikali ya nchi hiyo kutokana na janga la virusi vya Corona. Majina yao ni kama yafuatavyo;

1. Ramadhan Salum Juma.
2. Abdulkarim Yahya Mgeleka.

Jambo zuri na la kupendeza ni hili kuwa vijana wetu wawapo huko masomoni wamekuwa wakifanya vizuri sana darasani na hata kwa upande wa Nidhamu pia wamekuwa mfano mzuri na hivyo kuweka taswira njema ya chuo chetu nchini humo.

JAMIA PICNIC –SAFARI ZA MAFUNZO

Pamoja na majukumu mengi na mazito ya chuo, wanachuo pamoja na viongozi wamekuwa wakitumia fursa chache wanazopata kutembelea angalau mara moja kwa mwaka maeneo muhimu kama vile mbuga za wanyama nk. Kwa shabaha ya kujifunza mambo mbalimbali ya muhimu katika jamii. Na katika mwaka huu wa 2020 ziara hiyo ilifanyika katika moja ya Hoteli kubwa na maarufu hapa Morogoro iitwayo Highland na kuwashirikisha wabashiri wa mikoa.

KIKAO CHA WABASHIRI WA MIKOA

Miongoni mwa matukio makubwa yaliyojiri hapa chuoni, ni kufanyika kwa kikao cha wabashiri wa mikoa yote hapa nchini pamoja na Ameer sahib. Ndio kusema kuwa tumebahatika kuwa wenyeji wa ugeni huo mkubwa kabisa na wenye Baraka. Wakiwa hapa chuoni, wageni hao walishiriki katika hafla ya uwekaji wa jiwe la msingi wa shule yetu ya Sekondari ambapo mgeni rasmi alikuwa Mh. Ameer Jamaat. Na pia walishirikiana nasi katika Jalsa Seeratun Nabiy^{saw}, matukio hayo yote yalirushwa kupitia vyombo vya habari vya Abood Media –yaani Radio na Televisheni.

MAADHIMISHO YA SIKU YA MUHIMU KATIKA JAMAAT

Kwa kawaida katika idara yetu huwa tunaadhimisha siku zote muhimu kwa mujibu wa historia ya Jamaat. Lakini kutokana na mlipuko wa virusi vya Corona, mwaka huu wa 2020 hatukuweza kukamilisha ratiba hii na badala yake tulifanikiwa tu kuadhimisha Jalsa ya Yaumul Muslih Mau'ud r.a na Yaumul Khilafat.

CHANJO YA VIRUSI VYA CORONA

Kwa mujibu wa maeleezo ya Hazrat Khalifatul Masihil khaamis atba wanafunzi waliobaki Jamia katika likizo ya Corona, waalimu pamoja na familia zao wote walipatiwa chanjo hiyo, msimamizi wa mpango huo Sheikh Azeez Shahzad sahib alifanya jitihada za dhati kuhakikisha kuwa wote tunapata chanjo hiyo tena kwa mtiririko maalum. Pia idara yetu ya Jamia ilifanikiwa kugawa chanjo hiyo katika mikoa mbalimbali.

DARASA KATIKA MWEZI MTUKUFU WA RAMADHAN

Kwa fadhila za Allah na kwa maelekezo ya Amir Sahib katika mwezi mtukufu wa Ramadhan, Masheikh na waalimu wetu wa Jamiah walipata fursa ya kutoa darasa ambalo lilikuwa likirushwa atika mitandao ya kijamii.

MATUKIO MBALIMBALI YA JAMIAH KATIKA MITANDAO YA KIJAMII NA KATIKA M.T.A

Ukaribu uliopo baina ya chuo chetu na wanahabari, umerahisisha kurushwa kwa habari za matukio mbalimbali yanayofanyika hapa chuoni.

Matukio hayo ni kama vilke maadimisho ya siku ya mwana aliyeahidiwa, siku ya Masih aliyeahidiwa, siku ya Ukhalifa, Seeratu_nnabiyyin n.k. Pia habari za matukio hayo huchapishwa katika Gazeti letu la Mapenzi ya Mungu kwa lugha ya Kiswahili na Al-fazal international kwa lugha ya kiurdu. Pia baadhi ya habari hizo hurushwa katika channel yetu ya M.T.A AFRICA.

MISAADA MBALIMBALI KWA JAMII

Kwa upande wa ujirani mwema wa jamii, wanachuo pamoja na waufunzi wamekuwa na kawaida ya kutoa misaada mbalimbali sawa na uwezo kwa jamii yenye uhitaji. Sifa hii njema imejenga hali ya utangamano na jamii inayotuzunguka.

BAADHI YA KAZI ZILIZOFANYIKA MWAKA HUU

Miongoni mwa kazi muhimu zilizofanyika mwaka huu 2020 ni kuweka tiles za matofali ya mapambo kama zinavyoonekana, na hivyo kupunguza ada ya mavumbi na matope.

Na kazi nyingine ni ukarabati mkubwa uliofanyika katika nyumba ya mkuu wa chuo. Haya yote yamefanyika kwa shabaha ya kuboresha na kuimarisha mandhari ya mazingira yetu.

DARASA LA KUHIFADHI QUR'AN TUKUFU

Darasa hili la Hifdh linaendelea vizuri, katika darasa hili watoto hupokelewa muda wowote, hivyo tuitumie fursa hii kuwashajiisha wazazi kuleta kuleta watoto kwa shabaha hii.

ORODHA YA MAJINA YA WAHITIMU

Mheshimiwa Amiir Sahib, ifuatayo ni orodha ya majina ya wahitimu ambao hivi punde utawapa vyeti vya:-

Salim Omar - kutoka Kenya.
Mohammed M. Nyamawi - kutoka Kenya.
Shukuru Suleiman.
Hashim A. Ntenje.
Rashid Meja.
Shabaan Yunus.
Shuaib Issa - kutoka Malawi
Ibrahim Ally - kutoka Congo DRC na
Rajab Ibrahim – kutoka Congo DRC.

MUHTASARI WA RIPOTI YA SHULE

Kwa fadhili na Baraka za Allah, shule yetu ya Ahmadiyyah pre/primary school imeendelea kufanya vizuri katika nyanja zote, kuanzia darasani na maboresho ya miundo mbinu.

BAADHI YA KAZI ZILIZOFANYIKA KTK SHULE

Miongoni mwa kazi mpya zilizofanyika ni ujenzi wa darasa moja ambalo limeshakamilika. Darasa hilo litaongeza chachu ya kufundisha na kujifunza kwa ajili ya kudhibiti magari na bodaboda ambao walikuwa wakihatarisha usalama wa wanafunzi na hata waalimu pia.

Zaidi ya hayo, madarasa matatu ya zamani {ya kwanza kujengwa} yamefanyiwa ukarabati mkubwa ikiwa ni pamoja na uweka sakafu mpya n.k.

Kazi nyingine iliyofanyika ni uboreshaji wa mfumo wa ulipaji ada, ambapo sasa wazazi na walezi wa wanafunzi hutakiwa kulipa ada kupitia bank. Hatua hii imesaidia sana kutatua changamoto mbalimbali.

Kama inavyojulikana kuwa shule yetu haipo kibiashara, bali pia hujihusisha katika kutoa huduma, na kwa kuzingatia hilo, wanafunzi 130 katia ya 340 wanapata punguzo la ada.

Uongozi wa shule pia umeongeza idadi ya waalimu na kufikia kumi na nne, hatua hii nikatika kuinua na kuboresha iuwango cha elimu katika shule yetu.

Mkurugenzi wa shule ambaye pia ndiye mkuu wa Chuo cha Jamiah Ahmadiyyah Sheikh Abiid Mahmood Bhatty Sahib anatoa shukrani za dhati wa Masheikh na waalimu wa chuo cha Jamiah Ahmadiyyah, waalimu wa shule na wafanyakazi wengine, mbashiri wa Morogoro na wale wote waliochangia kwa namna moja au nyingine katika kufikia mafanikio haya.

Lakini shukrani zake maalumu na za pekee zinaenda kwa Mheshimiwa Amir Sahib ambaye muda wote amekuwa karibu naye katika kutoa ushauri wa kila namna na wa kufaa katika maendeleo ya shule. Anamwombea Allah ambariki na kumjaalia umri mrefu.

MWISHO

Mwisho mheshimiwa mgeni rasmi (Amir sahib) tunapenda kutoa shukrani zetu za dhati kabisa kwako kwa kuupokea na kuukubali mwaliko wetu.Hatuna malipo stahiki wako isipokuwa tunasema kwamba tunamwomba Allah azidi kukujaalia afya njema na kukurahisishia majukumu yako ya kila siu katika kutumikia Jamaat yake hii tukufu-Aamiin.

Unataka Kuanza Biashara?



Na **Mtaalamu Wetu**

Dhana hii imekuwepo kuwa watu wajiajiri na watarajiwa wa kujiajiri kudai hawakobeaheki yaani hawana mtaji?

Dhana ya mtaji wa Kukopa haijawahi Kumuwezesha yeyote Kuanza Biashara na Kufanikiwa
Biashara ya mwanzo zinachangamoto nyingi kwa sababu ya ugeni na uzoefu na network yako kuwa ndogo sokoni
Changamoto na zingine humfanya mkopaji kushindwa Kufanya rejesho hivyo kuingiwa kwenye kufilisiwa
Mikopo inahitaji rejesho na Muda ambapo mara nyingi huwa hauendani na muda na rejesho la Biashara yako
Mfano umekopa Tshs. 5,000,000 kuanzisha Biashara
Na ikiwa huna chochote unahitajika Kulipa pango, Na gharama zote za kuanzisha na Bidhaa
Takriban 2m mpaka 3m zinaweza kutumika Kuwezesha kuanzisha Biashara yako
Hivyo Bidhaa utanunua za 2m mpaka 3m
Hizi bidhaa ndizo unazofanyia Biashara
Kumbuka marejesho yapo kwa 5m na sio 3m
Hivyo Faida itakuwepo ya 3m na Kufanya marejesho Kufanyika sehemu ya mtaji baada ya Muda hata kama umerejesha vyema Biashara yako itafilisika
Nini kifanyike
Anzisha Biashara kwa Mtaji wako mwenyewe kwanza
Au Kopa mtaji wa Marejesho yatakayoanzia baada ya Kufanya Biashara kwanza kisha baada ya Muda huo fanya maresho
Kopa pesa ya Kuanzisha Bashara ukiwa tayari Unabiashara nyingine ambayo ndio Msingi wa marejesho yako na Biashara yako mpya Ikilelewa. Mfano Mkulima anakopa kwa Biashara yake ya nguo au Mfanyakazi anakopa kwa mshahara wake au njia yeyote ya backup ya rejesho
Kopa mtaji wenye marejesho madogo na ya Muda mrefu ili Biashara yako uilee
N.k
Haya yote hayawezekani Ikiwa tu kama Utaanza leo kuweka AKIBA kwa Biashara ya Kesho
Uuza Baadhi ya Mali zako kuanzisha Biashara
Upate Msaada wa Mtaji kwa ndugu, Jamaa na Dini
Anzisheni VICOBA ambapo watakuwepo wanachama ambao hawatakopa ila wataweka pesa kwa Muda mrefu na wanachama dhaifu wakope na marejesho yafanyike kwa Muda mrefu au baada ya kufanya Biashara kwanza
Bank usipokuwa na chochote kama Dhamana ya Mali mfano nyumba hawakukopeshi. Bank usipokuwa na Chanzo cha Marejesho Hawakukopeshi.
Bank hukopesha Biashara zilizotayari kwenye mzunguko au wenye vyanzo vingine vya Marejesho nje ya hapo HAKUNA ATAKAYE KUKOPESHA NA HAKUNA ATAKAYE KUKUPATIA MTAJI
FAIDA ya mikopo ni Kupanua Biashara na sio HUNA KABISA MTAJI WENYEWE NDIO MKOPO.
Huwezi pata ila pia ukipata Hutaweza kufanya rejesho
Wabunge wengine kwa mfano hutafuta Ubunge kwa sababu ili wapate umbrella ya Kukopesheka
Kilimo mfano huwezi na hakuna atakaye kupa Mkopo mpaka Mazao yafikie kwenye Kusimama yaani Miche kujitegemea au kuanza kutoa matunda
Biashara ya Mwanzo Inahasara inayokadiriwa kuanzia asilimia 60%-100%
Hivyo Wakopeshaji wengi huhofia Kupoteza Pesa zao na wakidhubutu kukopesha huweka masharti magumu kuwezesha pesa zao zinarejesha
Vijana kama mnataka kujiajiri Hakika tafuteni namna ya Kujinasua ASIWADANGANYE MTU anaweza Kujiajiri hivi hivi
INAWEZEKANA KUJIAJIRI
Ikiwa Tunaweza kuanzia kwa Biashara ndogo tuenda tukipanda
Mwaka jana niliizinishiwa na Access bank Mkopo wa 10m siku ya kuenda kuchukua Nilighailisha kwa sababu nilipiga mahesabu ya marejesho nilajikuta sina ya kutosha na mahesabu yote yakaonyesha Watauza tu nyumba yangu nikaacha kuichukua licha ya kunipigia sana Nikaiacha hiyo pesa
Sio furaha Kukopa ila Kukopa ni jambo zuri likwa na Uhakika
Vijana kama hutaki kuanza kuchuuza nenda Kutafute AJIRA. AJIRA Hutafutwa bila mtaji wowote ila Akiba yako Maarifa yako Kichwani tu
Uzuri wa kuanza Biashara ndogo kwa wasomi wanafaidika kwa MALI BILA DAFTARI HUTUMIKA BILA HABARI
Kumbukumbu zingi za shughuli zake huzifadhi na Kujipatia Tafsiri sahihi
Biashara ina vitu viwili ambavyo vinatakiwa kufahamika ili kuifanya Ikuwe na iwe endelevu daima
Kwanza MTAJI na Pili Running Costs - Pesa ya Kuzungushia au Kuendeshea Biashara. Zote Wakati wote zinategemea moja isipo kuwepo moja huiangisha nyenzie
MTAJI hutumika kuanzisha Biashara na kununua vitu vya MTAJI. Mfano Biashara yako ni Ndizi hivyo Unatakiwa Daima kuwa na Pesa ya Kununua Ndizi ili Uuze na Vifaa vyake na mahali pa kufanyia Biashara ya Ndizi.
Katika Biashara Kunagharama za uendeshaji ambazo hazihusikani na MTAJI ila vikikosekana Biashara haifanyiki mfano Mshahara, Usafiri, Umeme, n.k
Katika Kundaa mtaji hakikisha siku zote

PESA YA BIASHARA = MTAJI + RUNNING COSTS ZAKO
Running Costs hupatikana mara nyingi kutokana na Faida hivyo hakikisha Faida yako Ipo ya kutosha ili Upate Matumizi yako na Kuwa na Akiba ya Biashara
500 = 300 (Consumptions) + 200 (Saving)
Saving ndio hulipa mishahara na Wakati mwingine Kuongeza Mtaji.
Hakikisha kwa maana hiyo Kila Wakati Unaongeza Faida kuliko hasara. Na tambua kila unapoongeza au Kupanua Biashara ndivyo unakuwa unaongeza Matumizi hivyo kushuka kwa Mapato Huatarisha Usalama wa biashara na kipindi hicho haraka PUNGUZA MATUMIZI ili yaendane na Kipato chako na bila shaka hata muundo wa biashara hubadilika kwa Kufunga Baadhi ya Biashara na kupunguza wafanyakazi na gharama zote zisizo za lazima

Maisha ya Mtume Muhammad *saw*



Kutoka uk. 1

Allah, Muhammad*saw*. alikuwa akijua namna ya kufanya kazi, hakuwa akijua kujivunia kazi yake.
Baada ya ufunuo huu alikwenda kwa Hadhrat Khadija r.a. akiwa na uso uliofadhaika na athari za hofu zikidhihirika kwake. Hadhrat Khadija akauliza Nini kimetokea? Naye akaeleza tukio zima na akasema: Mtu dhaifu kama mimi nitawezaje kuubeba mzigo huu? Hadhrat Khadija akasema: Kallaa Wallaahi maa yukhziikal Laahu Abadan, innaka latasilur Rahma watahmilul kalla wataksibul ma'aduuma wa tukriud dhwaifa wa tu'iinu 'alaa nawaaibil haqqi (Bukhari bab badaul wahyi). Yaani: Kwa haki ya Allah, Allah Hakukuteremshia Maneno haya ili usifanikiwe na Mungu Apate kukutelekeza. Allah Anawezaje kufanya hivyo? Kwani wewe ni Yule uwatendeaye wema ndugu na jamaa na kubeba mizigo ya wale walio wanyonge wasio na msaada wowote. Wewe wazistawisha tena khulka zile zilizokwisha toweka katika jamii yetu. Unawakirimu wageni na kuwasaidia watu kwenye matatizo yao ya kweli. Je Mungu Anaweza kumuingiza majaribuni mtu wa aina hiyo?
Kasha (Bi Khadija) akaenda naye kwa binamu yake aliyeitwa Waraqa bin Naufal aliyekuwa ameshabadili dini na kuwa Mkristo. Yeye alipolisikia tukio hili basi mara moja akasema: Umeterenmkiwa na Malaika Yule Yule aliyeteremka kwa Musa. Kana kwamba alikuwa akiashiria kwenye bishara iliyomo ndani ya Kumbukumbu la Torati mlango wa 18 aya ya 18.
Habari hii ilipowafikia mabwana Zaid, aliyekuwa mtumwa aliyeachwa huru na Mtume*saw*. akiwa wakati huona na umri wa miaka 25 au 30 hivi, na Ali, mtoto wa baba yake mdogo, aliyekuwa wakati huo na umri wa miaka 11, wote wawili wakamuamini mara moja.

HADHRAT ABU BAKAR AMWAMINI MTUME WA ALLAH*saw*.

Abubakar r.a., rafiki wake wa tangu utotoni, aliyekuwa ameenda nje ya mji, alipoingia tu mjini sauti hii ikaanza kuingia masikioni mwake kwamba rafiki yako amekuwa mwehu. Anadai kwamba malaika amemteremkia kutoka mbinguni na kuanza kuongea naye. Abubakar mara moja akaenda kupiga hodi nyumbani kwake. Alipofungua mlango (Hadharat Abubakar r.a.) akamuuliza kuhusiana na ukweli wa mambo. Mtume*saw*., kwa ajili ya kuchelea kutomtelezesha rafiki yake wa tangu utotoni, akataka kutoa ufafanuzi. Abu Bakar akamzuia na kusema: Mimi nijibu hivi tu kwamba je wewe umetangaza hivi kwamba Malaika wa Mungu walikujia na kuanza kuongea nawe? Akataka tena kutoa maelezo, lakini Abubakar r.a. akasisitiza na kusema ulijibu tu swali langu bila ya kusema chochote.
Alipotoa jibu la kukubali, basi Abubakar akamwambia: Shuhudia kwamba Mimi Ninakuamini na kasha akasema: Ewe Mtume wa Allah. Kama ungetoa dalili basi ungeihafifisha imani yangu. Yule aliyeyaona maisha yako anaweza kuwa na haja ya kuona dalili nyingine yoyote ya ukweli wako.

JUMUIYA NDOGO YA WAAMINIO

Hii ilikuwa ni Jumuiya ndogo tu iliyoweka msingi wa Islam. Mwanamke mmoja aliyekuwa tayari ameshafikia umri wa uzee, mtoto wa miaka 11, Kijana aliyekuwa mtumwa aliyeachwa huru asiyekuwa na kwao na aliyekuwa akiishi kwa wengine ambaye hakuwa na familia yoyote, rafiki aliyekuwa kijana na mwenyewe aliyedai kupata ufunuo. Hili lilikuwa ndio kundi lile dogo lililotokeza kwenye uwanja wa ukafiri ili kueneza nuru duniani. Watu walipolisikia jambo hili wakaanza kucheka. Wakaanza kukonyezana wakiashiria kwamba hawa watu wamekuwa wehu. Msifadhaishwe na maneno yao, bali yasikilizeni na muyafurahie.
Lakini haki ikaanza kudhihirika kwa shani yake ya juu kabisa na sawa na bishara ya Nabii Isaya (Amri juu ya amri, amri juu ya amri, Sheria juu ya sheria, sheria juu ya sheria (Isaya: 28:13) ikadhihirika. "Hapa kidogo na kule kidogo" na "Lugha ya kigeni" ambayo hapo kabla Waarabu walikuwa hawaitambui.
Allah, Akaanza, kwa kupitia Muhammad*saw*., kuongea na Waarabu. Mioyo ya vijana ikaanza kutetemeka, miili ya watafutao ukweli ikaanza kusisimka. Kidogo kidogo, ndani ya sauti zao za kukejeli, kudhihaki na kukashifu, yakaanza pia kuibuka maneno ya kupendezwa na kuvutiwa. Kikundi cha watumwa, vijana na wanawake waliodhulumiwa kikaanza kujumuika kwake, kwa sababu ndani ya sauti yake wanawake walikuwa wakiona matumaini ya kupata haki zao. Watumwa walikuwa wakisikia ilani ya uhuru wao. Vijana walikuwa wakizihisi njia zilizofunguka za matumaini makubwa makubwa na za kimaendeleo.

UPINZANI WA VIONGOZI WA MAKKA

Wakati, ndani ya sauti za kukejeli na kukashifu, zilipoanza pia kusikika sauti za kuvutiwa na kusifia, basi wakuu wa Makka wakafadhaika, hofu ikaanza kuzalika ndani ya mioyo ya viongozi. Ndipo wakajumuika na kushauriana na kuandaa mipango. Na badala ya kukejeli na kukashifu, ikaamuliwa utolewe ushauri wa kufanya dhulma, ukatili, ukali na kukata mahusiano na yakaanzwa kutekelezwa dhidi yao (waaminio).
Sasa Makka, ikawa imeshachukua uamuzi wa dhati wa kupambana na Islam. Sasa "madai yaliyokuwa yakisemwa kuwa ni ya uwendawazimu" yakawa yanaonekana kuwa ni ukweli wenye kuendelea. Yakawa yanajidhihirisha kuwa ni hatari kwa siasa za Makka, hatari kwa ajili ya dini ya Makka, hatari kwa ajili ya utamaduni wa Makka na hatari kwa ajili ya mila na desturi za Makka.
Islam ikawa inaonekana ikitengeneza mbingu na ardhi mpya, ambapo kwa kuwepo kwa mbingu hiyo mpya na ardhi, mbingu ya zamani na ardhi ya zamani za Waarabu zisingeweza kudumu. Sasa suala hili halikuwa tena, kwa watu wa Makka, suala la kukejeli na kukashifu, sasa likawa ni suala la kufa na kupona.
Wakaikubali changamoto ya Islam na wakaikubali kwa roho ile ile, ambayo maadui wa manabii wamekuwa wakizikubali changamoto za manabii. Na wakawa tayari kutoa majibu ya dalili kwa njia ya upanga na mishale badala ya kutumia dalili. Wakaamua kujibu matakio mema ya Waislamu kwa wengine kwa kutoa matusi na lugha mbaya badala ya kutumia khulka njema.
Kwa mara nyingine tena vita kati ya Islam na kufuru ikaanza duniani. Kwa mara nyingine tena majeshi ya shetani yakawashambulia Malaika. Watu hawa wachache walikuwa na uwezo gani wa kukabiliana na watu wa Makka? Wanawake waliuawa kwa njia ya aibu, wanaume waliuawa kwa kupasuliwa msamba. Watumwa waliburuzwa juu ya mchanga wa moto na juu ya mawe yenye ncha kali hadi ngozi zao zikabadilika kutoka kwenye umbile la kibinadamu na kuwa katika umbile la wanyama.
Baadae sana, katika zama za ushindi wa Islam, wakati bendera ya Islam ilipokuwa ikipepea Mashariki na Magharibi, kulikuwa na mtumwa aliyesilimu mnamo siku za mwanzoni za Islam aliyeitwa Khubaab, ambaye mgongo wake ulikuwa wazi (bila nguo), basi wenzake wakaiona ngozi ya mgongo wake kuwa haifanani na ya mwanadamu bali iko kama ya mnyama. Walishtuka na kumuuliza 'una ugonjwa gani wewe?' yeye alicheka na kuwaambia: 'Huu sio ugonjwa, bali ni kumbukumbu ya wakati ule ambapo Waarabu walikuwa wakituburuza sisi watumwa tuliosilimu, juu ya mawe magumu yenye ncha kali kwenye mitaa ya Makka. Na waliendelea kutufanyia dhuluma hii. Haya ndio yalisababisha ngozi yangu iwe na umbile hili.

DHULUMA NA MATESO YA MAKAFIRI WA MAKKA KWA WATUMWA WALIOAMINI

Hawa watumwa waliomuamini Mtume*saw*. walitokana na mataifa mbali mbali, miongoni mwao walikuwemo pia Waafrika, kama vile Bilal r.a., walikuwemo pia Wayunani (Wagiriki) kama vile Suhaib r.a., pia walikuwemo miongoni mwao Wakristo kama vile Jabar r.a. na Suhaib r.a. Walikuwemo pia Washirikina kama vile Bilal r.a. na Ammaar r.a.
Mmiliki wa Bilal r.a. alikuwa akimlaza juu ya mchanga wenye joto kali na kuweka aidha mawe juu ya kifua chake au kuwateua vijana waliokuwa wakiruka ruka juu ya kifua chake. Bilal r.a. aliyekuwa na asili ya kiafrika, alikuwa ni mtumwa wa Umayya bin Khalf, aliyekuwa mmoja wa viongozi wa Makka. Umayya alikuwa akimchukua (Bilal ra) wakati mchana wa msimu wa joto kali na kumpeleka nje ya Makka na kumlaza juu ya mchanga wenye joto kali sana bila ya nguo. Na alikuwa akiweka mawe makubwa yenye joto kali juu ya kifua chake na huku akisema; Kiri uungu wa Lat na Uzza na dhihirisha kutengana na Muhammad saw. Bilal alikuwa akimjibu Ahadun Ahadun yaani Allah ni Mmoja tu, Allah ni Mmoja tu. Kila mara Umayya alipokuwa akilisikia jibu hili, akawa ndio anazidi kukasirika na kumfunga kamba shingoni mwake na kuwakabidhi watoto watukutu na kusema kwamba mchukueni huyo na kumburuza juu ya mawe yaliyoko kwenye mitaa ya Makka, ambapo matokeo yake yakawa kwamba mwili wake ukawa unavuja damu kwa wingi, lakini juu ya hayo, akawa tu anaendelea kusema Ahadun Ahadun yaani Mungu ni mmoja, Mungu ni mmoja tu, Mungu ni Mmoja tu.
Muda mrefu baadae, wakati Allah Alipowapa Waislamu amani huko Madina, wakati walipoweza kufanya ibada kwa uhuru, basi Mtume*saw*. akamteua Bilal r.a. kutoa adhana (huko Madina). Mtumwa huyu wa kiafrika alipokuwa akitoa adhana kwa kutamka As hadu an laa ilaaha illal lah badala ya

Endelea uk. 10

Bustani ya Washairi

MOYO EPUKA KIBURI

1. Kwako ndiko kimbilio, Ya Ilahi ya Swaburi,
Sikiza changu kilio, ona nilivyo hakiri,
Nipe langu hitajio, kiniepuke kiburi,
Moyo epuka kiburi, kiburi maangamio.
2. Kiburi maangamio, moyo epuka kiburi

Ulishike nyenyekeo, uwe kama muhajiri
Upate maendeleo, upae kama tuyuri
Moyo epuka kiburi, kiburi maangamio.

3. Ewe moyo muungwana, kaa kimya tafakari
Kakuumba Subhana, u shani yake nzuri
Ila umnyonge sana, sitara yako kaburi
Moyo epuka kiburi, kiburi ndio laana

4. Muumba unamkana, Na Yeye ndiye Mahiri
Wasimama kwa mapana, kwa maringo na jeuri
Kwa matendo unanena, ni wewe ulo Jabari
Moyo epuka kiburi, kiburi ndio laana

5. Huwazi yako asili, ukapata tafakuri
Uli ni tone dhalili, kalihifadhi Qahari
Mara ukawa jamali, thamani shinda johari
Moyo epuka kiburi, kiburi ni ujahili

6. Akakupa na akili, ukwepe kila la shari
Kakukunjulia mali, nawe uitwe tajiri
Kisha Mola humjali, hata kusema shukuri
Moyo epuka kiburi, kiburi ni ujahili

7. Una tele wafuasi, na mwingi umashuhuri
Zang'aa zako libasi, za kufumwa kwa hariri
Kisha huna wasiwasi, lini kifo kitajiri
Moyo epuka kiburi, kiburi uibilisi

8. Mapambo wajinafasi, hali mcheza kamari
Mdomo mengi matusi, nani wa kumhadhari
Watamba kadamnasi, ni mimi ndimi hodari
Moyo epuka kiburi, kiburi uibilisi

9. Wajivunia elimu, yako haina dosari
Hujali hata nidhamu, Aliyoweka Kahari
Dharau na kulaumu, ndio yako desturi
Moyo epuka kiburi, kiburi wendawazimu

10. Mnyonge mwanadamu, omba Istighfari
Lipi lako la kudumu, hata vipi linawiri
Kweli hili hufahamu? kwamba dunia ghururi
Moyo epuka kiburi, kiburi wendawazimu

11. Moyo mbona unakera, kama umetanasari
Vipi wajipa ubora, hali mbora Sattari
Mbele Yake garagara, Akwite akusitiri
Moyo epuka kiburi, kiburi kubwa hasara

12. Mola akupe busara, umuabudu kwa ari
Akulinde na hasira, uishi kwa tahadhari
Kwani hasira hasara, na chanzo chake kiburi
Moyo epuka kiburi, kiburi kubwa hasara

13. Moyo epuka kiburi, moyo wangu tafakari
Baki kama msafiri, juu ya hii sayari
Zishike zote amri, kwa sala na kusubiri,
Moyo epuka kiburi, kiburi ni ukafiri

14. Ichunge yako nadhari, kwa uchungaji mahiri
Ujiwekee nadhiri, kutokilea kiburi
Hicho ni mtunda pori, mazao yake shubiri
Moyo epuka kiburi, kiburi ni ukafiri

15. Mioyo tumefanana, sisi sote mafakiri
Mkamilifu hakuna, ukimtoa Kahari
Kisha moyo wajivuna, hata hili hufikiri
Moyo epuka kiburi, kiburi ushirikina

16. Moyo wacha kujiona, moyo ishike hadhari,
Hata vipi ungenona, mbeleyo kuna hatari
ni mengi usoyaona, Mola kayaficha siri
Moyo epuka kiburi, kiburi ushirikina

17. Kiburi chako cha nini, moyo unacho kiburi
Wajua ghaibu gani, hebu fikiri vizuri,
Sema ni sekunde gani, mwisho wa yako safari
Moyo epuka kiburi, kiburi ndiye shetani

18. Waliopita zamani, ni wangapi majeuri
Akina Fir'auni, walohodhi makasiri
Anowaheshimu nani, ziwapi zao fahari,
Moyo epuka kiburi, kiburi ndiye shetani

19. Niufupishe utungo, urefu usikithiri
Mola ukinge maringo, ulete njema athari
usijepoteza lengo, kwa kuzingwa na kiburi
Moyo epuka kiburi, kiburi, ndio mungu wa uongo

20. Nifungulie milango, Ilojaa kila kheri
Vikuwe vyangu viwango, kuuenzi ushairi
Iiname yangu shingo, kwa toba na kudhukuri
Moyo epuka kiburi, kiburi, ndio mungu wa uongo

Sheikh Abdulrahman Mohammed Ame

MAJI YAMELOANA

1. Msishangae kwa nini, kilowesha kuloana
Ndo mambo ya duniani, kaza roho tena sana
Sisingizie majini, eti kuna kurogana
Maji tumeita mma, nyuma moto mbele kiza.

2. Utataja sana watu, wanaleta kauzibe
Kumbuka kuna wahutu, mwendo mzobe mzobe
Unahisi sio mtu, mbona hivi tujibebe?
Maji tumeita mma, nyuma moto mbele kiza.

3. Biashara haziendi, kazini wanafukuzwa
Hauuziki mtindi, kodi bado tunatozwa
Mambo kweli hayaendi, kwa kweli tumeshalizwa
Maji tumeita mma, nyuma moto mbele kiza.

4. Mama n'tilie leo, tumeshakoma ubishi
Ukoloni mambo leo, mgambo wa magumashi
Hela ndio kimbilio, ili ufanye mapishi
Maji tumeita mma, nyuma moto mbele kiza.

5. Watu wanaosomesha, maji yamekorogeka
Lazima kuhakikisha, madeni yanalipika
Kutwa kuchwa kukumbusha, wenye shule wanawaka
Maji tumeita mma, nyuma moto mbele kiza.

6. Na sisi tuliopanga, magonjwa yanalipuka
Kodi imetia nanga, wenyewe wanaitaka
Hakuna kuchonga ngenga, hesabu imekatika
Maji tumeita mma, nyuma moto mbele kiza.

7. Magonjwa yametuzonga, sio presha sio busha
Mitishamba tunagonga, hosipitali kupisha
Na dhiki imeshagonga, iko ndani 'meipisha
Maji tumeita mma, nyuma moto mbele kiza.

8. Milo mitatu hapana, bateji imepelea
Tunapambana mchana, usiku tunadowea
Mambo yamebana sana, hakika tumepotea
Maji tumeita mma, nyuma moto mbele kiza.

9. Kama wataka balaa, mkopeshe mtu pesa
Usije kusema khaa, mapema nimekudesa
Ndugu hawana chapaa, ukimpa kapangusa
Maji tumeita mma, nyuma moto mbele kiza.

10. Vikoba vinatuua, madeni hayalipiki
Watu wanakuna pua, mambo mikiki mikiki
Madeni yatatuua, maisha hayasomeki
Maji tumeita mma, nyuma moto mbele kiza.

11. Kwenu wauza chakula, msije mkakopesha
Watakuja watakula, ahadi watawavesha
Kwa kweli mambo ya kula, Mungu mwenyewe atosha
Maji tumeita mma, nyuma moto mbele kiza.

12. Kwenu wauza magenge, hifadhini ndoa zetu
Tusije kusema tunge, heshimuni hali zetu
Hata kikopa 'sifunge, hatujui kesho yetu
Maji tumeita mma, nyuma moto mbele kiza.

13. Mlioko masomoni, someni someni sana
Ya huku ya duniani, sisi bado twapigana
Siseme ya kazi gani, elimu ya mana sana
Maji tumeita mma, nyuma moto mbele kiza.

14. Na nyinyi wanasiasa, hatutaki mazoea
Kama ubunge 'mekosa, fanya jambo la mbolea
Kalime hata kilosa, muweze jitegemea
Maji tumeita mma, nyuma moto mbele kiza.

15. Kama ni mwisho tayari, machache nimekumbusha
Namshukuru Kahari, mwaka ameufupisha
Nabaki ninasubiri, pendera kupeperusha
Maji tumeita mma, nyuma moto mbele kiza.

Abdallah Kalindima
#CHUMACHAKAVU
Nachingwea

UZALENDO.

Mimi ni Mtanzania, Mzalendo wa Taifa,
Tena ninajivunia, Kwa kila hali na sifa,
Taifa ta tumikia, Kama Baba wa Taifa,
Tanzania nakupenda, Daima sito kutenda.

Abubakary Abdallah Mwita.
Mkurya halisi.

RAZAKI

Yeye ndo mgawa riziki, Huruzuku kwa mafungu
Pindi tupatapo dhiki, Na kughubikwa machungu
Tusisahau huyu rafiki, Mtibu yote machungu
Nakushukuru razaki, Mtufaa kila hali

Watupa tustahilicho, So kila kile tombacho
Tugawapo bila choyo, Wongeza kipunguacho
Twaafiki unenayo, Na turadhi upendacho
Nakushuru razaki, Mtufaa kila hali

Shunda Mshundia Wana
Daluni, Tanga
+255656557721
Email: shunda267@gmail.com

PENGO KAMA PENGO.

Kifo chaleta huzuni, kwandugu na marafiki,
Haijulikani lini, wala hakitabiliki,
Ajuae ni manani, yeye ndie mmiliki,
Pengo umetuachia, Hakuna wa kuziba.

Yatililika machozi, pale nikifikiria,
Safari hii ni njozi, leo umetangulia,
Tumeumbwa jozi jozi, na sisi tutafatia,
Pengo umetuachia, Hakuna wa kuziba.

Ulionyesha dhamira, waqfu ulijitoa,
Haukuwa na hasira, ukaikacha dunia,
Mola awape subira, jamaa na familia,
Pengo umetuachia, Hakuna wa kuziba.

Saliana Ramadhani Higiro

TUMIA NAFASI

Maisha ni mzunguko, ulipo kweko tatoka,
Wengine walikokweko, wewe huko utafika,
Kila siku badiliko, mwisho mauti tafika,
Tumia nafasi uko, sijutie ikitoka.

Masihi Omary stambuli(Kisagwa)

Hawapo wasiri wangu, wote wamekwenda ng'ambo
Nimebaki peke yangu, baki kuimba nyimbo
Navumilia machungu, peke yangu na makumbo
Hii rehema ya Mungu, Sina budi kushukuru

Mahmood Hamsin Mubiru (Wa Mamba)

Seremala

Seremala mmoja alikuwa tayari kustaafu, na akamwambia mkuu wake juu ya mipango yake ya kuondoka na kwenda kuishi maisha ya raha pamoja na mke wake. Angeukosa mshahara wake wa mwezi huo, angeweza kusubiria, lakini alihitaji kustaafu.

Mhandisi alisikitika kuona mfanyakazi mzuri namna yake akiondoka, basi akamuomba seremala kutengeneza nyumba moja tu zaidi kama ombi lake binafsi.

Seremala akasema sawa, lakini kadri ya muda ilikuwa rahisi kuona kwamba moyo wake haukuwa katika kazi ile. Akafanya kazi ya stadi mbovu na alitumia malighafi dhaifu. Ilikuwa ni namna mbaya kumaliza kazi yake ya muda mrefu vile.

Seremala alipomaliza kazi yake, mhandisi akaja kuikagua nyumba. Akakabidhi funguo ya mlango wa mbele kwa seremala. "Hii ni nyumba yako," mhandisi alisema. "Ni zawadi yangu kwako."

Seremala alishtushwa! Aibu gani hii? Kama tu angejua alikuwa anatengeneza nyumba yake mwenyewe, angeitengeneza kiupekee kabisa.



Vivyo hivyo na kwetu pia. Tunajenga maisha yetu, kila siku, aghalabu tukiweka juhudi kidogo kuliko uwezo wetu katika mjengo. Kisha kwa mshtuko tunagundua tunabidi tuishi kwenye nyumba tuliyojenga.
Kama tungeweza kujenga tena, tungefanya kwa ufanisi sana. Lakini hatuwezi kurudi nyuma...
Wewe ni seremala wa maisha yako. Kila siku unagongelea msumari, unaweka ubao, au kusimamisha ukuta. Tabia zako na machaguo unayofanya leo hujenga "nyumba" yako ya kesho...

TAFUTA MANENO

Yatafute maneno hapo chini kwa kuyazungushia na Penseli

W	A	T	H	A	M	U	D	I	J	M	I	Z	T	I	R	Q	N	Q	Y
L	G	D	W	G	P	I	F	K	A	B	F	B	V	M	S	L	M	Q	X
T	T	L	T	R	T	G	U	W	M	W	T	B	R	I	F	L	K	M	K
D	R	M	K	I	X	F	I	A	M	V	B	T	H	P	T	H	A	R	J
K	L	B	K	L	I	L	H	O	C	H	R	H	P	K	E	E	K	M	R
T	R	I	Y	L	U	D	I	M	A	N	A	B	I	I	U	N	N	J	N
W	S	J	I	Y	W	N	B	Q	U	I	J	R	V	V	B	M	D	D	Z
M	X	D	N	N	I	C	H	G	H	S	X	N	Z	M	A	W	D	A	O
R	A	A	V	M	L	N	N	A	G	M	T	V	P	U	D	O	B	T	M
S	Y	P	A	M	P	I	R	Z	L	A	W	F	M	H	H	N	D	M	S
N	A	A	L	T	B	A	T	C	X	I	K	H	D	A	I	G	V	P	H
Y	W	H	W	M	J	M	H	M	T	L	M	K	U	M	R	O	L	Q	U
R	N	W	A	A	W	K	P	A	W	X	C	Q	Z	M	I	Z	N	A	K
L	C	M	H	B	F	V	B	R	J	U	R	P	U	A	F	O	M	X	U
L	M	S	Y	W	A	W	V	D	B	I	J	L	R	D	U	I	K	B	R
B	I	N	A	D	A	M	U	M	Z	N	R	I	I	P	T	H	Y	Y	A
K	H	I	F	A	D	H	I	T	D	T	L	A	Z	A	Y	Y	X	W	N
V	J	T	Z	H	V	U	K	R	I	S	T	O	Y	A	N	D	F	J	I
V	H	K	H	A	T	A	M	A	N	N	A	B	I	Y	Y	I	N	V	F
H	H	P	V	Y	N	G	K	M	S	A	M	A	H	A	T	C	G	N	N

UNGANISHA NUKTA

Unganisha nukta ili upate picha moja iliyokamilika.



Upishi wa Keki ya Tende

Na **Mtandao**



Mahitaji
Unga/ngano - 2 cups
Mayai - 4
Sukari - 1 cup
Siagi - 1cup
Maziwa fresh - 1cup
B. powder - 2 tsps
B.soda - 1/2 tsp
Vanila esence - 1tsp
Tende iliyotolewa mbegu - 1cup

Maelekezo
Anza hatua kwa hatua.

Saga tende na maziwa ktk blender mpaka ilainike, Weka pembeni.
Chukua bakuli weka sukari na siagi piga kwa kutumia mwiko mpaka iwe kama cream nzito kisha weka mayai moja baada ya moja.
Kisha weka mchanganyiko wa tende endelea kuchanganya.
Kisha mwisho utaweka unga, B.p na B.s na vanila.
Pika ktk ovena kama taratibu ipikwapo cake.

Ni tamu kwa kahawa..

ASEMAVYO MASIHI ALIYEAHIDIWA AS

Acha Kiburi

Mtakapoiacha tabia ya Kiburi, basi mahala pake pazibwe kwa Unyenyekevu na Unyonge, mtashambuliwa tena na kiburi. Hivyo, kuweni wanyenyekevu kwa sababu hii ndio njia Aipendayo Allah. Hata yeye mwenyewe alifikisha Unyenyekevu mpaka kiwango cha juu kabisa usio na kifani, ndipo Allah Akifurahi Akamwambia kwa kumfunulia Njia zako za Unyenyekevu zikampendeza.

Hazrat Aqdas Masih Mau›udi as anasema: Ninasema kwa Ukweli kabisa kwamba siku ya kiama, baada ya Shirki hakutakuwa na balaa zaidi ya Kiburi. Hili ni balaa ambalo humdhalilisha Mwanadamu Duniani na Akhera. Rehema ya Allah humzunguka kila yule anayeamini umoja wa Mungu isipokuwa mwenye Kiburi. Hata Shetani alikuwa akisema kuwa anaamini umoja wa Mungu, lakini kwa kuwa ndani ya kichwa chake mlikuwa na Kiburi, na alipomtazama Adam, aliyekuwa akipendwa na Allah, kwa mtazamo wa dharau na kumkosoa, basi, akaangamizwa na kongwa ya laana ikavikwa shingoni mwake. Hivyo Dhambi ya kwanza iliyomuangamiza milele Mtu ilikuwa ni Kiburi. (Aina Kamalate Islam, Rubani Khazaain, J.5, uk. 598).

Tena anasema: Kama kwa jiha yoyote mnacho Kiburi au tabia ya kujionyesha au kujisifu au uvivu, basi ninyi si kitu kinachostahili kukubalika. Isije mkachukua mambo machache na kujidanganya kuwa mmeshafanya mlichotakiwa Kufanya, kwa sababu Mungu Anataka mapinduzi Kamili yatokee ndani ya dhati yenu. Yeye Anataka kwenu mauti fulani ambayo baada yake Atawahuisheni. (Kashtie Nuh, Ruhani Khazain, J. 19, uk. 12)

DARASA LA QUR'AN TUKUFU

UMUHIMU WA SALA ZA JAMAA

Na **Musa Salum Mgeleka -** 0717 504 690

تَكَادُ ٱلسَّمَٰوَٰتُ يَتَفَطَّرۡنَ مِن فَوۡقِهِنَّۚ وَٱلۡمَلَٰٓئِكَةُ يُسَبِّحُونَ بِحَمۡدِ رَبِّهِمۡ وَيَسۡتَغۡفِرُونَ لِمَن فِي ٱلۡأَرۡضِۗ أَلَآ إِنَّ ٱللَّهَ هُوَ ٱلۡغَفُورُ ٱلرَّحِيمُ

Ni karibu mbingu zipasuke toka juu yao, na Malaika hutukuza kwa kumsifu Mola wao na huwaombea msamaha waliomo ardhini. Angalieni! hakika Mwenyezi Mungu ni Msamehevu, Mwenye huruma. [Surat Ash-Shura 6]

MBINGU ni Paa 2:23 na Paa huangalia vyema athari mbaya za mazingira na kustawisha maendeleo mbalimbali. Mazingira yanaharibiwa basi Paa huharibika katika mazingira kama hayo ufanisi wa Paa huondoka. Manufaa ya mbingu huondoka na kusalia Fadhili na Rehema za Allah moja kwa moja. Rehema ya vitu vilivyofanywa Rehema inapoondoka, Rehema inayobakia ni Rehema ya Allah ya moja kwa moja isiyopitia kwa vitu. Rehema hii ni Kubwa na ndio hunusuri vitu vyote vinavyozungukwa na Hatari. Anguko, ajari, maafa, ugomvi, hitilafu hutokea ikiwa Rehema ya Allah ikikosekana.

Aya hii imeeleza namna tatu ambazo zikitumika au zinavyotumiwa huwezesha kuwepo kwa Nusura ya shida zote;

1 Kumtukuza kwa kumsifu Mwenyezi Mungu. Kumtukuza Allah kulimuokoa Nabii Yunus a.s asibaki kwenye tumbo la Samaki 37:140-144

2◎ Kuombea msamaha waliomo ardhini. Ndio njia ya Rehema 71:11-13

3◎ Mungu ni Msamehevu, Mwenye huruma. Ambao hawafanyi makosa hali wa wakijua 3:136-137 hali hii imeendelea kuinusuru dunia na watu wake. Makosa mengi ni ya ujinga au kusababishiwa hivyo huruma ya Allah huwakumba.

Mola wetu, Usitutwike tusiyoyaweza, na Utusamehe, na Utughofirie, na Uturehemu; Wewe ndiwe mlinzi wetu; basi Utusaidie juu ya watu makafiri. Amin

TANZIA

Wakati tunaenda mtamboni tumepokea habari za kifo cha Mzee Ubwa ambaye kwa miaka amekuwa 'Auditor' wa Jamaat Ahmadiyya Tanzania, Sisi ni wa Allah na Kwake Tutarejea.

Tunaahidi InshaAllah katika toleo lijalo kueleza maisha ya Mzee Ubwa

Mhariri

MATUKIO KATIKA PICHA



Wanajamaat wa Ibushi wakimsikiliza Amir na Mbashiri Mkuu katika ufunguzi wa msikiti



Kambi ya Malezi Ruvuma kwa ajili ya Atfal, na Nasrat



Washiriki wa Qaideen Forum katika picha ya pamoja na Amir na Mbashiri Mkuu baada ya ufungaji



Picha ya pamoja Amir Jamaat na wanatawi wa Igungumalo baada ya ufunguzi wa msikiti



Sehemu ya Ansarullah waliohudhuria katika Ijtimaa ya Taifa ya Majlis Ansarullah Ahmadiyya 2020



Amir na Mbashiri Mkuu akihutubia majirani wa Kitonga katika mkutano wa ujirani mwema



Amir na Mbashiri Mkuu akihutubia Semina ya viongozi wote Dar es salaam



Picha ya pamoja ya wahudhuriaji wa semina ya Malezi Tanga



Kambi ya Malezi Iringa kwa ajili ya Atfal, na Nasrat



Kambi ya Malezi Iringa kwa ajili ya Atfal, na Khuddam huko Mtwara

Waqar-e-Amal - Mbeya Mjini

"usafi ni sehemu ya Iman"

Tawi la Mbeya mjini limefanikiwa kufanya Waqare Amal leo tarehe 27 siku ya jumapili 2020 huko wakisafisha na kurekebisha eneo la shule na barabara yake.

Waqare Amal iliendelea kwa muda wa masaa mawili kuanzia saa 7:30 hadi 9:30. Allah Azibariki juhudi hizi. Aamin





Kambi ya Malezi kwa ajili ya Naasiratul Ahmadiyya

Tandhim ya Naasiratul Ahmadiyya ilifanya mafunzo ya malezi ya watoto wa kike wenye umri chini ya miaka 15 mkoani Dares Salaam.

Maisha ya Mtume Muhammad *saw*



Kutoka uk. 5

Ash hadu an laa ilaaha illal Lah, basi watu wa Madina, waliokuwa hawazijui hali zake, wakaanza kucheka. Siku moja Mtume*saw*. aliwasikia watu wakicheka wakati Bilal alipokuwa akitoa adhana, basi aliwageukia watu na kusema: Ninyi mwaicheka adhana ya Bilal, lakini Allah huko kwenye arshi, Hufurahi kuisikia adhana ya Bilali. Alikuwa akiashiria hivi kwamba: Ninyi mnaona hivi tu kwamba yeye hawezi kutamka shin sawasawa, lakini mna nini ndani ya shin au sin. Mungu Anafahamu kwamba wakati alipokuwa akilazwa bila nguo juu ya mchango wenye joto kali na madhalimu walikuwa wakirukaruka juu ya kifua chake wakiwa na viatu vyao na walikuwa wakiuliza Je umeshapata somo sasa hivi au la? Basi yeye alikuwa akiutangaza umoja wa Allah kwa lugha yake isiyokuwa fasaha kwa kutamka Ahadun Ahadun na kutoa uthibitisho wa uaminifu wake na uimara wa imani yake na itikadi yake ya Tauhid. Hivyo As hadu yake ilikuwa na thamani zaidi kuliko Ash hadu za watu wengi.

Hadhrat Abubakar r.a. alipoiona dhulma hii dhidi yake, basi akamnunua kwa mmiliki wake na kumuachia huru. Hali kadhalika Hadhrat Abubakar r.a. aliwaachia watumwa wengine wengi tu kwa namna hii. Miongoni mwa watumwa hao, alikuwemo pia Suhaib aliyekuwa tajiri sana. Huyu alikuwa akifanya biashara na alikuwa akifahamaika kuwa miongoni mwa watu wa maana wa Makka. Lakin i juu ya yote haya, kwamba yeye alikuwa ni tajiri na pia alishakuwa huru, Makureishi walikuwa wakimpiga hadi kuzimia. Mtume*saw*. alipohamia Madina, basi baadae Suhaib naye akatamani kuhamia Madina. Lakini watu wa Makka wakamzuia kwa madai kwamba wawezaje kuchukua mali zote hizi ulizozichuma hapa Makka. Sisi hatutakuruhusu uondoke Makka. Suhaib akasema kama niziache mali zote hizi, je mtaniruhusu niondoke? Wao wakaliafiki jambo hili, naye akawakabidhi mali zote watu wa Makka na kwenda Madina akiwa mikono mitupu, na akaenda kwa Mtume*saw*. Mtume*saw*. akasema: Suhaib! Biashara yako hii imekuwa na faida kuliko ile ya mwanzo. Yaani hapo awali ulikuwa ukichuma fedha kwa kuuza bidhaa, lakini sasa umeipata imani badala ya fedha.

Wengi miongoni mwa watumwa hawa walikuwa imara (kiimani) kwa ndani na kwa nje, lakini baadhi yao ulidhihirika udhaifu kwa nje. Hivyo wakati fulani Mtume*saw*. alipita kwa Mtumwa fulani aliyeitwa Ammaar na kuona kwamba alikuwa akilia huku akijifuta machozi. Akamuuliza: Kuna nini ewe Ammaar? Ammaar akajibu: ewe Mtume wa Allah, hali ni mbaya sana! Waliendelea kunipiga na kunitesa na hawakuniachia hadi walipoitoa kinywani mwangu kauli dhidi yako na ya kuwakiri miungu (yao). Mtume*saw*. akauliza; Lakini ulikuwa unahisi nini moyoni mwako? Akajibu; moyoni nilikuwa naihisi imani isiyotikisika. Mtume*saw*. akasema: Kama moyo ulikuwa na utulivu juu ya imani, basi Allah Atausamehe udhaifu wako.

Makafiri walikuwa pia wakiwatesa sana baba yake aliyeitwa Yasir na mama yake aliyeitwa Sumaiyya. Hivyo siku moja wakati wawili hao walipokuwa wakiteswa, Mtume*saw*. alipitia hapo. Aliyaona masaibu ya wote hao wawili na moyo wake ukajaa uchungu. Akawaambia, Swabran aala Yaaswir fa inna mauw'idakumul Jannatu yaani Fanyeni subira enyi ukoo wa Yaasir, Allah Ameshawaandalia Pepo. Na bishara hii ikatimia ndani ya siku chache tu, kwa sababu Yasir aliaga dunia kutokana na kipigo. Lakini juu ya haya makafiri bado hawakutosheka na wakaendelea kumdhulumu mkewe kikongwe Sumaiyya. Kwani siku moja Abu Jahal alipandwa hasira na kumpiga mkuki wa nguvu pajani uliopenya hadi tumboni na akakata roho kwa maumivu makali.

Zanbira pia alikuwa ni mjakazi fulani ambaye Abu Jahal alimpiga hadi akapofuka. Abu Faqih alikuwa ni mtumwa wa Safwan bin Umayya. Mmiliki wake na familia yake walikuwa wakimlaza juu ya ardhi yenye joto kali na kuyaweka mawe makubwa yenye joto kali juu ya kifua chake hadi ulimi wake ukawa unatokeza nje. Hali hii hii ilikuwa ndio ya watumwa wengine.

Bila shaka dhulma hii ilikuwa nje ya uwezo wa mwanadamu, lakini wale watu waliokuwa wakidhulumiwa, kwa dhahiri walikuwa ni binadamu na kwa ndani walikuwa ni malaika. Kurani haikuwa tu inateremka kwenye moyo na masikio ya Mtume*saw*., bali Allah Alikuwa pia Akiongea ndani ya mioyo ya watu hao. Na hakuna dini yoyote iwezayo kustawi hadi ndani ya mioyo ya waumini wake wa mwanzoni itoke sauti ya aina hiyo ya Allah, wakati wanadamu walipowatelekeza, wakati ndugu na jamaa zao walipowaepuka, basi Allah Alikuwa Akiwaambia ndani ya mioyo yao kwamba: Mimi ni pamoja nanyi, Mimi ni pamoja nanyi. Na dhulma zote hizi zikawa ni raha kwa ajili yao. Matusi yakageuka kuwa maombi. Mawe yakashika nafasi ya dawa ya kuchua. Upinzani ukazidi kuendelea lakini imani nayo ikazidi kuongezeka. Dhulma ikafikia kilele chake, lakini uaminifu nao ukavuka mipaka yote iliyotangulia.

DHULMA KWA WAISLAMU WAUNGWANA

Hata waislamu waliokuwa huru nao pia hawakupata dhulma pungufu. Waheshimiwa wao na wakubwa wa familia zao nao pia walikuwa wakipatiwa aina mbali mbali za usumbufu. Hadhrat Uthman r.a. alikuwa ni mtu mwenye umri wa takriban miaka arobaini na alikuwa ni mtu tajiri. Lakini juu ya hayo, wakati Makureishi walipoamua kuwafanyia dhulma Waislamu, basi baba yake mdogo aliyeitwa Hakam, alimfunga kamba na kumpiga barabbara. Zubair bin Awam alikuwa ni kijana shujaa sana. Katika zama za ushindi za Islam, yeye alithibitika kuwa Jenerali madhubuti. Naye pia alisumbuliwa sana na baba yake mdogo. Alikuwa akimfunga ndani ya jamvi na kumuweka juu ya moshi ili asipate kuvuta hewa na kisha kumwambia: Je sasa utaepukana na Islam au la? Lakini alikuwa akizivumilia shida hizo na kutoa jibu hili kwamba: Mimi siwezi kuukataa ukweli baada ya kuutambua.

Hadhrat Abu Dhar alikuwa ni mtu wa kabila la Ghaffar. yeye alisikia kwamba huko Makka kuna mtu amedai kuwa ametoka kwa Allah. Yeye akaja Makka kufanya uchunguzi. Basi watu wa Makka wakampoteza na kumwambia kuwa : Muhammad mbona ni jamaa yetu, sisi twafahamu kwamba yeye amefungua duka. Lakini Hadhrat Abu Dhar ra hakujiepusha na dhamira yake. Hivyo akafanya mipango mingi na hatimaye akawasili kwa Mtume*saw*. Mtume*saw*. alimweleza mafundisho ya Islam naye akaipokea Islam. Alimwomba Mtume*saw*. ruhusa kwamba: Je kama sintowaambia watu wangu kwa muda fulani kuhusiana na Islam, je kuna dhara yoyote. Mtume*saw*. akamwambia kwamba kama utanyamanza kwa siku chache tu, basi hakuna dhara. Akarejea kwa watu wa kabila lake pamwe na ruhusa hii na akadhamiria moyoni kwamba nitajirekebisha kwa muda fulani kisha nitaudhihirisha Uislamu wangu.

Alipokuwa akipita ndani ya mitaa ya Makka, akaona kwamba viongozi wa Makka wakiutusi Uislamu. Wakati huo huo dhamira yake ya kuisitiri imani yake kwa siku kadhaa ikatoweka na akajikuta akilazimika kutangaza mbele ya kikao kile kwa kusema: Ash hadu an laa ilaaha illaLaahu wa ash hadu anna Muhammadan Rasuulul Lah yaaani mimi ninashudia kwamba Allah ni Mmoja Asiye na mshirika yeyote na ninashuhudia kwamba Muhammad ni mja wake na mtume wake.

Iliposikika tu sauti hii kwenye kikao hiki cha maadui, watu wote wakasimama ili kumpiga na wakampiga hadi akazimia, lakini hata hivyo wadhalimu hawakujizuia na wakaendelea kumpiga. Wakati huo huo, baba mdogo fulani wa Mtume*saw*. aliyeitwa Abbas, ambaye hadi wakati huo alikuwa bado hajasilimu, aliwasili hapo na kuwafahamisha watu na kusema kwamba misafara yenu ya nafaka huja kwa kupitia kwenye maeneo ya kabila la Abu Dhar. Kama watu hao watakasirika basi Makka itakufa kwa njaa. Ndipo watu hao wakamuachia. Abu Dhar alipumzika siku moja na siku ya pili akawasili kwenye kikao kile kile. Kwenye vikao hivyo suala la kuongea dhidi ya Mtume*saw*. ni jambo la kila siku. Alipokwenda kwenye Kaaba basi ni maneno hayo hayo yaliyokuwa yakiendelea. Akasimama tena na kuitangaza itikadi yake ya Tauhid na tena watu hao wakaanza kumpiga, na hali hii ikaendelea kwa siku tatu na baada ya hapo akaelekea kwenye kabila lake.

Itaendelea toleo Lijalo

TANZIA

Tarehe 07/12/2020, tuliondokewa na Dokta Iddi Ibrahim Mwanga na huku nyuma akituachia maumivu makubwa. Sisi ni wa Allah na Kwake tutarejea.

Dokta Mwanga katika miaka ya sabini, themanini na tisini alilitumikia gazeti hili kwa kutoa makala za kuelimisha. Katika toleo lijalo tutaeleza InshaAllah juu ya maisha ya Daktari huyu aliyeamini kwamba ili tiba ya mwili iwe na maana ni lazima pia utibu roho.

Kwa nini Biblia Ni Jibu Wanamkana Nabii Issa kuwa Si Yesu?

Inaendelea Kutoka toleo lililopita

Hoja ya Pili

Biblia ni Jibu wakiendela kumkataa Isa wanasema Waislam huwa wanapinga hoja mbalimbali kuhusu imani ya kikiristo na hasa kufa na kufufuka kwa Bwana Yesu. Wakasema Waislam hutuma andiko la ndani ya Qur'an Sutar An Nisai 4:157 kwa ajili ya kusema kwao kuwa sisi tumemuuwa Masihi Isa Mwana wa Mariam, hawakumuuwa wala hawakumsulubu, walakini walibabaishiwa mtu mwingine. Mwisho wa kunukuu aya.

Wanaendelea kusema kundi hilo la Biblia ni Jibu kuwa hapo ndipo Yesu na Isa ikidaiwa ni mtu mmoja. Wakati sio kweli. Kwani ndani ya Biblia Yesu amesema Imenipasa kwenda Yerusalem na kuuwawa na siku ya tatu kufufuka. (Mathayo 16:21-23) wakati kauli hiyo inapingana na maneno ya Yesu. Mwisho wa kunukuu

Hoja wanayotumia Biblia si Jibu sio hoja, kwani Qurani inachopinga ni kauli ya Mayahudi sio kauli ya Yesu. Kwani Mayahudi ndio waliodai kumuuwa Yesu.

Hivyo Quran inapinga Isa hakuwa Nabii wa uongo lakini. Pia huyo ni Yesu aliyetoroshwa utotoni. Je Yesu aliyekulia mle mle Jerusalem naye alisema atakufa? Au ndio kusema Biblia nzima Yesu alisema neno moja tu la kufa na siku ya tatu kufufuka? Je ndani ya Quran Tukufu kuna sehemu yeyote ambayo Isa alisema juu ya kufa kwake au kutokufa kwake? Bila shaka hakuna. Kwani ndani ya Quran Allah Nduye Anayetoa taarifa kuwa ile ilikuwa kauli ya Mayahudi. Hivyo kama Yesu atakuwa alikufa kweli siku tatu, huyo atakuwa siye Yesu wa Quran kwani nimeishaonyesha kuwa wapo Mayesu wawili.

Je katika Biblia hakuna Yesu ambaye hakufa? Maana ni kweli katika Biblia yupo Yesu aliyesema atakufa na siku ya tatu atafufuka. Na yupo Yesu aliyesema atakuwa kama Yona ndani ya tumbo la nyangumi. Je Yona alikufa? Tusome kitabu cha Torati kinasema nini kuhusu Nabii wa uwongo?

Torati 21:22-23:- Akiwa mtu ametenda hambi impasayo kufa, akauwawa nawe ukamtundika juu ya mti. Mzoga wake usikae usiku kucha juu ya mti; lazima utamzika siku hiyo hiyo kwani alietundikwa amelaniwa na Mungu.

Hii ndio habari inayopingwa na Quran juu ya Isa a.s. kwani tunajua Yesu alitumwa na Mungu lakini Mayahudi hawakutaka kumsadiki na walimuona ni Nabii wa uongo. Kuhakikisha kuwa ni mtu alielaaniwa. Na kwa imani hiyo ya Kiyahudi ni kweli hawezi kuwa Issa kwani Ussa ni yesu asielaaniwa.

Maana yangu ni kwamba Yesu aliyesema atauwawa na siku ya tatu atafufuka huyo hawezi kuwa Isa bin Mariam wa Quran, huyo ni Yesu mwingine. Yesu aliyelaaniwa.

Je Mathayo 12:39-40 huyo hawezi kuwa Isa? Andiko linasema kizazi kibaya cha zinaa kinataka ishara hakitopata ishara isipokuwa ishara ya Yona. Maana kama vile Yona alivyokuwa siku tatu katika tumbo la nyangumi mchana na usiku siku tatu hivyo ndivyo Mwana wa Adam atakavyokuwa siku tatu mchana na usiku katika moyo wa nchi. Je Yona katika tumbo la samaki alikuwa mfu?

JE, UKWELI HALISI WA SURA 4:158 NI UPI?

Ukweli ni kwamba hoja ya kubadilishiwa mtu mwingine hapo haipo na sio hoja ya Kiislam. Kwani Isa sie Nabii wa kwanza kuteswa na hata kilugha haikubaliki na kubadilishiwa mtu. Kwani shubiha ni mfanano wa aina fulani.

Kwa kuwa Mayahudi wao shida yao ilikuwa ni kumuuwa Yesu hivyo hapo SHUBIHA ni mfanano wa kifo yaani Mayahudi walimuona kama mfu.

Na jambo lingine ni:- SWALABA – sio mateso. Swalaba ni tendo la aina yake.

Kuuwawa kwa kupigiliwa juu ya mti Kuvunjwa mifupa na kutolewa mafuta ya katikati ya mifupa yaani supu.

Je kwa ufafanuzi huo kuna tofauti ipi na ukweli wa Biblia? Aya imeonyesha kuwa Isa bin Mariam hakuuwawa msalabani yaani wamakataluhu – hawakumuua, walakin shubbiha lahu - lakini walifananishiwa na kifo, yaani walimuona kuwa kudhani ni mfu. WAMASWALABUHU :- Hawakumvunja kumtoa supu yaani mafuta ya miguuni na mikononi. Hivyo ndivyo ilivyotokea kwa Yesu ambaye ni Isa hata ndani ya Biblia.

Nitatoa aya mbili tu za Biblia zatosha kuonyesha uwiano wa aya hiyo ya Quran juu ya Yesu na ni moja toka Agano la Kale na moja toka Agano Jipya. Hebu tuanze na agano la kale kitabu cha Zaburi.

Zaburi 34:19-21:- Mateso ya mwenye haki ni mengi lakini bwana humponya nayo yote huifadhi mifupa yake yote, haukuvunjika hata mmoja. Uovu utamuua asie haki.

Kifungu cha pili ni:-

Yohana 19:32-36:- Basi askari wakaenda, wakamvunja miguu wa kwanza na wapili aliyesulubiwa pamoja naye. Lakini walipomjia Yesu na kuona ya kuwa ameishakufa hawakumvunja miguu. Lakini askari mmoja alimchoma mkuki ubavuni na mara ikatoka damu na maji. Nae alieona ameshuhudia, na ushuhuda wake ni kweli. Nae anajua anasema kweli ili nanyi mpate kusadiki. Kwa maana hayo yalitukia ili andiko litimie. Hakuna mfupa wake uliovunjwa.

Kama nilivyosema aya hizo mbili zinatosha kuoanishwa na aya hiyo ya Quran. Aya ambayo Biblia ni Jibu wanaonesha kuipinga eti haiwezi kumuhusu Yesu. Wakati Zaburi ilionesha kabla kuwa Yesu atapata mateso lakini hatokufa. Je Quran ikisema wamakataluhu – yaani hawakumuuwa vipi asiwe Yesu? Je Quran ikisema walakin shubbiha lahu – yaani alifananishiwa kwao kama maiti – kosa litakuwa wapi kuwa siye Yesu? Mbona askari alipotaka kumvunja mifupa iliafe akamkuta ameisha kufa? Je alimuua tena? Halafu anasema alichoma mkuki ikatoka damu na maji. Je aliyekufa damu na maji huendelea kufanya mzunguko katika mishipa? Je hamuoni kama alizimia mzimio uliofanana na kifo? Mwisho anasema hawakuvunja mifupa ili litimie andiko la hautovunjika hata mfupa wake. Je mbona andiko hilo limeonesha vyote viwil havitompata? mateso hayatamuuwa

hautavunjika mfupa wake

kwa maelezo hayo ni lazima iwe wamaakataluhu wa maswalabuhu – yaani hawakumuuwa Yesu wala hawakumvunja vunja. Huyo aliyetabiriwa na kutolewa habari hizo na bwana Yohana ndiye Isa, il ahuyo aliyekufa na kufufuka siku yatatu hawezi kuwa Isa bin Mariam. Na hakuwa ni wazi wapo Mayesu wawili ndani ya Bibia. Kwa mujibu huo itakuwa sio busara kuihukumu Quran pasipo kumkataa Yesu huyo wa Yohana aliyetabiriwa katika Zaburi 36.

Hoja ya Tatu

Itaendelea toleo lijalo

Masahaba Walioongoka: Hadhrat Uthman[ra]

Kutoka uk.12

Makka kwa niaba ya Waislamu, pamoja na ujumbe kutoka kwa Mtukufu Mtume[saw] ulioelekezwa kwa wakuu wa Makka. Wakati Hazrat Uthman[ra] alipokwenda, alikutana na wakuu wa Makka na akawasilisha ujumbe wa Mtukufu Mtume[saw] kwao. Walakini, wakuu wa Makka walibaki wakaidi na wakasema kuwa hawatakubali Waislamu kuingia, hata hivyo walisema kwamba watamruhusu yeye Hazrat Uthman[ra] azunguke Ka'bah. Hazrat Uthman[ra] alisema angewezaje kufanya hivyo, wakati Mtukufu Mtume[saw] alikuwa anazuiliwa kuingia Makka. Kwa hivyo, Hazrat Uthman[ra] alianza kufanya maandalizi ya kurudi kwenye kambi ya Waislamu, hata hivyo watu wa Makka walimzuia kuondoka.

Juu ya hili, habari za uwongo zilienea kwamba Hazrat Uthman[ra] ameuawa shahidi. Baada ya kusikia haya, Mtukufu Mtume[saw] aliwakusanya masahaba wote na kuchukua kiapo kutoka kwao, kwamba sasa watasonga mbele na hawatarudi nyuma, hata ikiwa inamaanisha kutoa maisha yao. Mtukufu Mtume[saw] alinyoosha mkono wake na masahaba wakaweka mikono yao juu yake. Kisha, Mtukufu Mtume[saw] aliweka mkono wake mwingine juu ya mikono yao, na akasema kwamba huu unawakilisha mkono wa Hazrat Uthman[ra], kwani kama angekuwepo, bila shaka angeshiriki katika kiapo hiki. Kiapo hiki kinajulikana kama Bai'at-e-Ridhwan. Kuhusu kiapo hiki imetajwa katika Kurani Tukufu kuwa:

Kwa hakika Allah Amewawia radhi waaminio walipofungamana nawe chini ya mti, na Aliyajua yaliyomo mioyoni mwao. Basi Akateremsha utulivu juu yao, na Akawalipa ushindi wa karibu. (48:19).

Baada ya kusikia juu ya kiapo hiki, wakazi wa Makka waliogopa, na mara moja wakasema kwamba makubaliano yafanywe, hata hivyo Waislamu hawapaswi kuruhusiwa kuingia hadi mwaka unaofuata; na kwa hivyo walimpeleka Suhail bin Amr kwa Mtukufu Mtume[saw] ili kukamilisha masharti ya mkataba. Kwa hivyo, mkataba uliandikwa, ambao unajulikana kama Mkataba wa Suluhu ya Hudaibiyah.

Khalifa mtukufu[atba] alisema kwamba ataendelea kuangazia matukio kutoka kwenye maisha ya Hazrat Uthman[ra] baadaye.

Wito wa Maombi

Khalifa mtukufu[atba] aliikumbusha tena Jumuiya juu ya maombi haswa kwa hali ilivyo nchini Pakistan, ambapo Waahmadiya hawana salama hata ndani ya kuta za nyumba zao. Polisi wako chini ya ushawishi wa maulvis (mamula). Khalifa mtukufu[atba] alisema kuwa kuna polisi wenye tabia nzuri ambao wanasema kwamba wanalazimika kutenda kwa njia ambayo wameagizwa na wakuu wao. Khalifa mtukufu[atba] aliomba kwamba Waahmadiya wabaki salama kutoka kwa watu kama hao na kuwawezesha kuishi kwa urahisi. Khalifa mtukufu[atba] alisema kwamba - Inshaallah, ikiwa tunaendelea kuomba, basi hivi karibuni tutaona hatima mbaya ya watu hawa. Khalifa mtukufu[atba] aliomba kwamba tuwe na uwezo wa kuendelea na maombi yetu katika suala hili.

The First Muslim Newspaper in Swahili Language since 1936

MapenziyaMungu

JAM.I-RAJ 1442 AH | JAN-FEB 2021 | TABLIGH 1400 HS

Kutoka Hadithi za Mtume Mtukufu^{saw}

Mtume^{saw}. alisema, Mwenye kumwangalia mjane na maskini atapata thawabu ya Haji na Jihadi **(Bukhari, Muslim).**

Makhalifa Walioongoka: Hadhrat Uthman^{ra}

Katika hotuba ya Ijumaa ya tarehe 29/01/2021 iliyotolewa Masjid Mubarak, Islamabad, UK; baada ya Tashahhud, Ta'awwudh na Surat Faatihah, Khalifa Mtukufu, Hadhrat Amir ul Mu'miniin, Mirza Masroor Ahmad^{atba} ('Ayyadahullahu Ta'ala Bi-Nasrihil Aziiz') alisema kwamba ataendelea kuangazia matukio kutoka kwenye maisha ya Hazrat Uthman^{ra} na vita ambavyo alishiriki.



Masjid Mubarak: Hadhrat Khalifatul Masih V^{atba} huhutubia Ijumaa kwa waaminio tokea na kurushwa duniani kote kwa njia ya satelaiti.

Vita vya Badr

Khalifa mtukufu^{atba} alisema kwamba Hazrat Uthman^{ra} hakuweza kushiriki kidhahiri katika vita vya Badr kwani mkewe Hazrat Ruqayyah^{ra} alikuwa mgonjwa. Kwa hivyo aliamriwa na Mtukufu Mtume^{saw} kubaki nyuma na kumtunza. Baadaye, Mtukufu Mtume^{saw} alimjumuisha katika mgawanyo wa ngawira za vita, na kwa hivyo aliweza kushiriki katika njia hii.

Vita vya Ghatafan

Khalifa mtukufu^{atba} alisema kwamba wakati Mtukufu Mtume^{saw} alipoelekea Ghatafan, alimteua Hazrat Uthman^{ra} kama naibu wake huko Madina, na kwa hivyo Hazrat Uthman^{ra} hakushiriki katika Vita vya Ghatafan pia. Khalifa mtukufu^{atba} alielezea historia ya vita hivi, na jinsi makabila mengine ya Banu Ghatafan walivyokusudia kushambulia Madina. Mtukufu Mtume^{saw} aligundua mipango yao, na kwa hivyo ili kupunguza tishio, Mtukufu Mtume^{saw} alisafiri na jeshi kuelekea Banu Ghatafan. Baada ya kujua juu ya kuwasili kwa Mtukufu Mtume (saw), makabila mbali mbali yalikimbia kuelekea milimani ambapo walijificha. Ingawa vita haikupiganwa, tishio la kushambuliwa kwa Madinah halikupungua.

Tukio Wakati wa Vita vya Uhud

Khalifa mtukufu^{atba} alisema kwamba Hazrat Uthman^{ra} alishiriki katika Vita vya Uhud. Khalifa mtukufu^{atba} alisema kuwa wakati wa vita, kulikuwa na Waislamu wengine ambao, waliposikia habari za uwongo kwamba Mtukufu Mtume^{saw} aliuawa shahidi, na baada ya shambulio la kushtukiza lililofanywa na Abu Sufyan na vikosi vyake, waliondoka kwenye uwanja wa vita. Imeandikwa kwamba Hazrat Uthman^{ra} alikuwa miongoni mwa wale ambao waliondoka kwenye uwanja wa vita. Khalifa mtukufu^{atba} alinukuu aya ifuatayo ya Kurani Tukufu kuhusu wale waliokimbia:

Hakika wale waliorudi nyuma miongoni mwenu siku ambayo majeshi mawili yalikutana, kwa yakini Shetani ndiye aliyewatelezesha kwa sababu ya baadhi ya waliyoyachuma, na bila shaka Allah Ameshawasamehe. Hakika Allah ni Msamehevu, Mpole sana. (3:156).

Khalifa mtukufu^{atba} alielezea visa kadhaa kutoka kwenye vita vya Uhud, akielezea jinsi Maquraishi walivyoeneza habari za uwongo kwamba Mtukufu Mtume^{saw} aliuawa shahidi mikononi mwao. Baada ya kusikia haya na kuvunjika moyo kabisa, kulikuwa na masahaba wengine, ingawa walikuwa wachache kwa idadi, ambao waliondoka kwenye uwanja wa vita na kurudi kuelekea Madina. Walakini kwa sababu ya uaminifu wao, Mungu Mwenyezi alitaja katika Kurani Tukufu kuwa walisamehewa. Kulikuwa na kundi lingine la masahaba, ambao waliposikia habari hii ya uwongo hawakurudi Madina lakini kwa sababu ya huzuni kubwa ya habari hii walivunjika moyo na kuelekea upande mmoja wa uwanja wa vita. Kulikuwa na kundi la tatu ambalo, licha ya kusikia habari hii, liliendelea kupigana. Baadaye, mara tu wale wa vikundi viwili vya kwanza waliposikia kwamba Mtukufu Mtume^{saw} kweli alikuwa hai, mara moja walirudi kwenye uwanja wa vita. Imeandikwa kwamba Hazrat Uthman^{ra} alikuwa sehemu ya kundi la pili ambaye hakurudi Madina, lakini alielekea upande mmoja wa uwanja wa vita.

Mkataba wa Hudaibiyah

Khalifa mtukufu^{atba} kisha akataja matukio ya Hazrat Uthman^{ra} kuhusiana na Mkataba wa Suluhu ya Hudaibiyah. Khalifa mtukufu^{atba} alielezea kwamba Mtukufu Mtume^{saw} alikuwa ameona katika ndoto kwamba alikuwa akizunguka Kaaba, na kwa hivyo alichukulia kuwa inamaanisha kwamba anapaswa kusafiri pamoja na masahaba zake kwenda Umrah (hija ndogo). Ilikuwa ni mwezi wa Dhul-Qa'dah, mmoja wa miezi mitakatifu ambayo mapigano yalikuwa yamekatazwa, kwa hivyo Mtukufu Mtume^{saw} aliwaamuru masahaba zake kwamba panga zao zibaki kwenye ala zao. Na hapo Mtukufu Mtume^{saw} alisafiri kuelekea Makka na masahaba zaidi ya elfu moja na mia nne.

Njiani, Mtukufu Mtume^{saw} alisimama huko Dhul-Hulaifah ambapo yeye na masahaba zake walivaa Ihram na Mtukufu Mtume^{saw} pia alimtuma sahaba wake mmoja kuelekea Makka, ili kupata habari na kuhakikisha kuwa watu wa Makka hawafanyi ufisadi wowote. Sahaba huyu alirudi akibeba habari kwamba watu wa Makka walikuwa na nia ya kuwazuia Waislamu wasiingie Makka na walikuwa tayari hata kupigana nao. Walikuwa hata wametuma kikundi kuwakamata Waislamu njiani. Kwa hivyo, Mtukufu Mtume^{saw} aliagiza kwamba hawapaswi kuchukua njia inayojulikana kuelekea Makka lakini washike njia tofauti ili kuepusha mzozo wowote.

Halafu, Mtukufu Mtume^{saw} na masahaba zake walisimama karibu na bonde la Hudaibiyah. Hapa mtu mmoja wa Makka alimweleza Mtukufu Mtume^{saw} kwamba wakuu wa Makka hawatamruhusu kamwe kuingia Makka na kwa hakika watapigana naye. Mtukufu Mtume^{saw} alisema kwamba yeye hakuwa na nia ya kupigana nao kabisa, bali alikuwa tayari hata kufanya mkataba nao. Alitoa hotuba ya kutoka moyoni ambayo ilimgusa sana mtu yule wa Makka aliyeitwa Budail, ambaye alisema kwamba atawajulisha na kujaribu kuwashawishi wakuu wa Makka. Hatimae wakuu wa Makka walishawishiwa na Chifu mmoja aliyeitwa Urwah bin Mas'ud na hivyo wakakubaliana na pendekezo hili. Chifu huyu alikwenda kwa Mtukufu Mtume^{saw} kwa niaba ya watu wa Makka.

Aliporudi Makka, Urwah alisema kwamba alikuwa ametembelea wafalme na viongozi wengi, lakini hajawahipo kuona mtu yeyote akiheshimiwa na kuenziwa, mithili ya vile masahaba wa Mtukufu Mtume^{saw} wanavyomheshimu na kumuenzi.

Halafu, Maquraishi walituma wawakilishi kwa Mtukufu Mtume^{saw} ili kujadili makubaliano. Mtukufu Mtume^{saw} pia aliamua kwamba mwakilishi wa Kiislamu pia apelekwe Makka, ili aweze pia kuwaelezea maoni ya Waislamu juu ya jambo hilo na kuwaelezea vizuri msimamo wao. Walakini, wakati akiwa njiani, ngamia wake alishambuliwa na kujeruhiwa, na ingawa watu wa Makka walitamani kumshambulia pia, walimwacha na kumfanya arudi kwenye kambi ya Waislamu.

Maquraishi kisha waliamua kutuma vikosi kuzunguka kambi ya Waislamu kwa siri, na baada ya kupata fursa, kuwashambulia Waislamu. Walakini, Mtukufu Mtume^{saw} alikuja kujua juu ya njama hii, na licha ya wao kufanya hivyo katika mwezi mtakatifu, Mtukufu Mtume^{saw} aliwasamehe.

Khalifa mtukufu^{atba} alisema kuwa kutokana na matukio haya, mtu anaweza kuona kiwango cha uvumilivu kilichoonyeshwa na Mtukufu Mtume^{saw} na hamu yake ya kudumu ya kustawisha amani.

Mtukufu Mtume^{saw} hakukatishwa tamaa na matukio haya yote, na akaamua kwamba mtu mashuhuri ambaye asili yake ilikuwa Makka atumwe ili kujaribu kuwasaidia wakazi wa Makka kuelewa nia ya kweli ya Waislamu. Kwa hivyo, Hazrat Uthman^{ra} alitumwa

Endelea uk 11